**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU,**
**TAWALA ZA MIKOA ZA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA KAHAMA**

***Unapojibu Tafadhali Taja:***

**Kumb.Na KMC/R.30/7/92** **07 Machi, 2026**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MKATABA

Halmashauri ya Manispaa ya Kahama kupitia Divisheni ya Afya, Ustawi wa jamii na Lishe na kwa kuzingatia Mwongozo wa Kitaifa wa kujitolea kwa Wataalamu wa Afya Mkurugenzi wa Manispaa Kahama anapenda kuwatangazia Wanachi wote wenye Sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Manispaa Kahama, kuomba nafasi za Mkataba kuanzia tarehe **07 Machi, 2026.**

### 1.0. *DAKTARI DARAJA II – NAFASI (05)*

### 1.0.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye Shahada ya Udaktari kutoka Chuo Kikuu kinachotambuliwa na Serikali waliohitimu mafunzo ya mazoezi katika kazi (Intership) yaliyoidhinishwa na Baraza la Madaktari Tanganyika (Medical Council of Tanganyika) na kusajiriwa kisheria na Baraza hilo.

### 1.0.2 KAZI NA MAJUKUMU YA DAKTARI DARAJA LA II

- Kufanya shughuli zote za matibabu Hospitalini zinazohusiana na magonjwa ya kawaida, magonjwa ya watoto, magonjwa ya akina mama na upasuaji wa kawaida na dharura.
- Kufanya kazi zote za kinga na afya ya jamii na kubuni mikakati ya kupambana na magonjwa yanayoambukiza.
- Kusimamia watumishi wodini na sehemu nyingine za kazi.
- Kutoa ushauri nasaha kwa wagonjwa na jamii kwa ujumla.
- Kufundisha wanafunzi wa Vyuo vya Uganga.
- Kufundisha na kuwaendeleza kitaaluma watumishi walioko kwenye hospitali.
- Kufanya utafiti kuhusu magonjwa na kuendeza matokeo ya utafiti kwa jamii.
- Kupanga, kufuatilia na kutathimini utoaji wa huduma za afya.
- Kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi.



Created with Photo-to-PDF One Click Converter. Download here: https://firehawk.ai/phototopdf
https://firehawk.ai/phototopdf/

### 1.0.3 NGAZI YA MSHAHARA TGHS E1

Kwa kuzingatia viwango vya mishahara ya Serikali katika ngazi ya **TGHS E1** kwa mwezi na kama ilivyoelekezwa katika Mwongozo wa Kitaifa wa kujitolea kwa Wataalamu wa Afya kwa waombaji wa nafasi za Mkataba watalipwa nusu Mshahara ya nafasi husika iliyotangazwa.

## 2.0. *MTEKNOLOJIA MIONZI DARAJA II (RADIOGRAPHER II) – NAFASI (02)*

### 2.0.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne/sita wenye Stashahada ya kwanza katika Fani ya Sayansi ya Mionzi (X-ray) kutoka katika sayansi ya Radiolojia na Mionzi (Radiographa) kutoka katika Chuo Kikuu cha Dar essalaam au chuo kingine chochote kinachotambuliwa na Serikali.

### 2.0.2 KAZI NA MAJUKUMU YA *MTEKNOLOJIA MIONZI DARAJA II (RADIOGRAPHA II)*

- Kufanya uchunguzi wa magonjwa kwa kutumia njia mbalimbali za Sayansi za Mionzi.
- Kutunza na kuhakikisha vifaa vya radiolojia vinafanya kazi vizuri
- Kusaidia madaktari katika tafsiri ya awali ya picha
- Kuchakata na kuhifadhi picha za radiolojia
- Kufanya matengenezo madogo ya vifaa
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

### 2.0.3 NGAZI YA MSHAHARA TGHS B1

Kwa kuzingatia viwango vya mishahara ya Serikali katika ngazi ya **TGHS B1** kwa mwezi na kama ilivyoelekezwa katika Mwongozo wa Kitaifa wa kujitolea kwa Wataalamu wa Afya kwa waombaji wa nafasi za Mkataba watalipwa nusu Mshahara ya nafasi husika iliyotangazwa.

## 3.0 MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE.

i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania ambaye ana umri wa miaka 18 mpaka 45

ii. Mwombaji aambatishe nakala ya Cheti cha kuzaliwa.



Created with Photo-to-PDF One Click Converter. Download here: https://firehawk.ai/phototopdf
https://firehawk.ai/phototopdf/

iii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya Wadhamini (referees) watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za Simu.

iv. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya Elimu na taaluma kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali, na vilivyothibitishwa na Wakili au Kamishna wa Viapo.

v. Testimonials, provision results, statement of results, havitakubaliwa

vi. Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE.

vii. Kwa waombaji wote wa nafasi ya **DAKTARI II** mnaelekezwa kuambatisha Leseni ilihuishwa.

viii. Waomabji waambatanishe picha moja passport size ya hivi karibuni

ix. Barua ya Maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kingereza.

x. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **14 Machi, 2026.**

xi. ***MUHIMU:*** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti, aidha anuani ya barua hiyo ielekezwe na kutumwa kwa;

Mkurugenzi wa Manispaa,
Barabara ya Boma,
S.L.P 472,
**KAHAMA – Shinyanga.**

xii. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioanishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**

***NB: Tanganzo hili linafuta tangazo la tarehe 06 Machi, 2026 lenye Kumb. Na. KMC/R.30/7/91"***

Imetolewa na

Masudi S. Kibetu
**MKURUGENZI**
**HALMASHAURI YA MANISPAA**
**KAHAMA**



Created with Photo-to-PDF One Click Converter. Download here: https://firehawk.ai/phototopdf
https://firehawk.ai/phototopdf/